

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



Mei 01, 2022

OFISI YA MKUU WA WILAYA,
S.L.P 02,
LUDEWA.

TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Waziri Waziri Kindamba leo Mei 01, 2022 amekua mgeni rasmi katika siku ya maadhimisho ya Wafanyakazi Duniani ambapo kimkoa yamefanyika katika Halmashauri ya Mji Makambako katika Uwanja wa Polisi Makambako.

Aidha Mhe. Waziri Kindamba wakati wa hutuba yake amewasisitiza Wananchi wa Mkoa wa Njombe kuendelea kuchukua tahadhari ya Maambukizi ya Ukimwi huku akiongeza kwa kuwasihi wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya UVIKO 19.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Waziri Waziri Kindamba amewaagiza waajiri wote mkoani hapo kujali masilahi ya Wafanyakazi na amesisitiza kwa kusema kuwa mwajiri anawajibu wa kupeleka sehemu ya mshahara wa Wafanyakazi wao katika mfuko wa (NSSF) Kama sehemu ya akiba yao baada ya kustaafu.

Katika maadhimisho hayo wamehudhuria viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndugu Sunday Deogratias.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

Chrispin B.Kalinga
Afisa Habari (W) Ludewa